# Learning by Ear 2009

## Media & Information

**Author: Hope Azeda**

**Redaktion: Ludger Schadomsky**

**Kisuaheli Traslation: Eric Ponda**

## EPISODE 1

| | |
|---|---|
| ***CHARACTERS:Wahusika*** | |
| **Announcer:** | **Male/female** |
| **"Young Junior"** | **Male, 15 years old** |
| **"Sister P."** | **Female, 16 years old** |
| **"Charlie"** | **Male, 18 years old** |
| **"Ezra":** | **Male, 22 years old. Brother to "Young Junior".** |
| **Askari:** | **Adult male** |

***INTRO/Scene Setting***

Hujambo na karibu kwa awamu nyingine ya mfululuzo wa vipindi vyetu vya Lerning By Ear "Noa Bongo Jenga maisha yako". Wakati huu tukizungumzia sekta ya habari na Mawasiliano.

Je, na uchu wa kuwa mtangazaji katika Televisheni? Au labda wewe ni shabiki wa redio na mpenzi wa wa burudani la Muziki? au

shabiki wa kutuma maoni kwa kutumia simu yako ya mkononi fursa hiyo inatokea?

Katika awamu hii ya vipindi vya Lerning By Ear, tutazungumzia kwa kina sekta hii ya habari na Utangazaji,Nini umuhimu wa sekta hii?, Na vipi mtu anaweza kuanzisha kituo cha habari? Au ni wapi unaweza kupata habari?.
Ungana nasi tunapokutana na wahusika wa katika kipindi hiki.

**Young Junior** : Mvulana wa umri wa miaka 15 mwenye busara, mwasisi wa kilabu ya Muziki ya vijana chipukizi "Dot.Com. music.Club yaani "DCC". Mbali na kuwa mwanamuziki mashuhuri pia azma yake ni kuendelea na masomo kutimiza ndoto kwamba siku moja ataweza kuanzisha gazeti lake na kuliita **"The Brain Drill".**

Kisha tuna **Sister P**, msichana wa umri wa miaka 16 mwenye sauti ya ninga. Ni muimbaji wa kutegemewa katika klabu hii ya Dot.Com, ingawa ndoto yake ni kwamba siku moja ataweza kuanzisha vipindi vya televisheni ili kuangazia vipawa vya wasichana na maisha wanayopitia. Vipindi ambavyo pia vitakuwa na kitengo cha mahojiano na mijadala ya ana kwa ana kwa jina "**The Me in Me"**

Ni msichana mwenye msimamo dhabiti na kamwe hapendi kuchezwa shere na wavulana kama itakavyobainika katika vipindi vitakavyofuatia.

**Charlie** Alizaliwa na kipawa cha uimbaji. Ari yake kubwa na kuimba kila anapopata fursa hiyo. Yeye pia ni muimbaji katika klabu hiyo ya Dot.Com na ndoto yake ni kuwa mtangazaji maarufu yaani DJ katika moja wapo ya vituo vya Redio

**Ezra** .ni mvulana wa umri wa miaka 22, mwenye umri mkubwa zaidi katika kundi hili, na ni kakake Young Junior na mwanafunzi wa taaluma ya uandishi wa habari katika chuo kikuu cha eneo hilo.

Yeye ni kipenzi wa Redio na mwenye ujuzi mwingi katika taaluma hii, kwani mbali na kusomea kazi hiyo pia ni mtangazaji katika kituo cha Redio chuoni mwake.Ezra pia husaidia kutayarisha vipindi. ikiwa ni pamoja na Muziki ambapo klabu ya Dot.Com pia inajiandaa kurekodi kanda yao ya kwanza. Lakini cha kusikitisha ni kwamba kituo cha utangazaji cha taifa kinakataa kucheza Muziki wao.

**Na hapo ndipo hadithi yetu inapoanzia**. …**TUKITUMAINI KUWA UTAFURAHIA!**

***SCENE 1 Youth centre***

| |
|---|
| ***SFX:*** *Aina mbali mbali ya michezo ikiendelea, huku mpira wa vikapu ukidundishwa mara kwa mara sakafuni, na kando kidogo ya ya uwanja huo wa vikapu kunauwanja wa kandanda ambako kundi la vijana wanaendelea kucheza. Wachezaji wanasikika wakiitana wanapoendeleakucheza .Sauti ya mtu akitembea na madirisha ya darasa hatimaye yakifungwa..* |

**1. Askari:** ***(Rough and scary voice)*** Hebu simama hapo….ngoja! Unafanya nini? Wewe huruhusiwi kufunga madirisha! Yafungue!.

**2. Sister P:** Ahha ***(breath of relief***)…Askari…! kwani unaniogopa. Twende mahala faragha.

**3. Askari:** Kufanya nini ?

**4. Charlie:** Sisi ni wanachama wa klabu ya Dot.Com. Tunataka kufanya mazoezi ya kuimba hapa. Jina langu ni Charlie!.

**5. Sister P:** Na mimi naitwa Sister P. Hiki hapa ni kibali kutoka kwa wahusika wakuu ***(SFX shuffling papers***)

**6. Askari:** Kwanini kibali kimekunjana hivi?… kwani kinakihifadhiwa katika mdomo wa mbuzi ?

**7. Charlie**: Haitatuchukua muda mrefu.Ni saa moja tu.

**8. Askari:** Saa moja tu na sio zaidi!

**9. Sister P**: Ehh Mungu, Charlie!…yule Askari ni mkali… anaroho ngumu kama chuma!. Kwani amekula nini mchana!….. maji au nini?

**10. Charlie**: Sister P, bora uanze mazoezi yako kuimba.

**11. Sister P**: (***starts singing***) ….***Dream On…Yeah Dream on…….***

***SFX: (Running footsteps and screaming/ laughing kids)***

**12. Askari:** ***(shouting and scolding)***

Nyinyi watoto..nikimshika nitamchapa kiboko!

(***Kids laugh so loud that Charlie ends up laughing himself, Sister P stops singing)***

**13. Sister P:** Aaaah…. Siwezi kuendelea kuimba!.

**14. Charlie:** Fuata shughuli yako.

**15. Sister P:** Shughuli gani sasa ? Kucheza kandanda….Mpira wa vikapu.. ya askari au makelele ya watoto? …Unacheka? Hebu twende studioni tukafanye mazoezi huko.Young Junior yuko wapi ? Amechelewa!.

**16. Charlie:** Watu wanajiuliza maswali mengi kuhusu kipawa na juhudi zetu za kuimba.

**17. Sister P:** Unasema nini wewe?

**18. Charlie:** Hebu fikiria juhudi zetu zote hizi, muda tunaochukua kutayarisha kanda yetu ya kwanza, kuiwasilisha kanda hii kwa kituo utangazaji cha

taifa ,…na kisha hadi sasa hatujasikia muziki huo ukichezwa.

**19. Sister P:** Ni kweli ... maana kila wakati unaposikisikiliza redio ya taifa, ni mahojianon tu….mahojiano!…matangazo ya vifo, taarifa zisizo na umuhimu, habari na kadhalika, …ni mambo yan kuchukiza sana! . Sijui kwanini Bibi yangu anapenda kusikiza redio hiyo. Kila mara utamkuta akisikiliza redio hiyo.

**20.Charlie:** Hali kadhalika Babangu!.Unapomkuta ameketi varandani katika kiti chake cha mbao,akinywa aina ya pombe aipendayo huku akisikiza stesheni ya taifa kpitia kiji-redio chake, utacheka!

.

***(takes a deep breath in and out)*** aaaaah… ni kama ambaye amefika peponi.
***(a bicycle bell rings)***

Young J. amewasili! Vipi bwana?

**21. Sister P:** Umechelewa..! .

**22. Young J:** Najua ***(not bothered***). Eheee nini kinachoendelea hapa , Sister P.?

**23. Sister P**: Hebu nenda huko, Young Junior!. Huna samahni? Tunaweza kwenda sasa ?

**24. Young J**: Ndio, lakini tusubiri dakika moja!. Ezra amesema atatuita akiwa tayari . Kwa sasa tunaweza kuendelea na mazoezi yetu.

**25. Sister P:** Lakini hapa kuna makelele sana. Ehe hebu tueleze nini kipya leo Young J?

**26. Young J:** Ehe! Umesikia kuhusu waendeshaji Pikipiki nchini Nigeria ambao hawataki kuvalia kofia rasmi za usalama na ili kuwakwepa Polisi wa trafiki wao huvalia mafuvu ya ***Malengelenge***?

***(All: Laugh)***

**27. Charlie:** Huo ni unacheksha sana! hupata wapi habari hizi?

**28. Young J:** Kutoka vituo vya redio za kimataifa. Kwani wewe Charlie husikizi redio hizi au pia wewe hujigandisha katika redio ya taifa tu?

**29. Sister P:** Huo ndio ubaya wa Redio. Habari huwa zinapeperusha na upepo tu, huwezi kuzihifadhi!.

**30. Young J:** Hii ndio sababu nataka kuanzisha gazeti langu, Sister P.

**31. Charlie:** Kwanza gazeti ndilo baya zaidi Young J. Unafikiri nani atasoma gazeti hilo?

**32. Sister P:** Na utaliitaje?

**33. Young J:** ***BRAIN DRILL !*** Sitaki majina kama vile *THE SUN or THE TIMES.* ***(excited***) Jamii yetu imechoshwa na matangazo na vipindi vinavyopeperushwa na redio yetu ya Taifa. Na ili kuwachemsha bongo watu wetu,tunahitajika kuanzisha gazeti hili la ***"Drill".***

| | |
|---|---|
| **SFX:** | (***Phone rings***) |

**34. Sister P**: Huyo ni Ezra, Young Junior? Nampenda sana, ni mtu mwenye busara kuliko wewe.

**35. Young J:** Sister P, Unataka kusema limekutoka tu ?

**36. Sister P**: ***(Sister P laughs)*** Shhhhhh shhhh

**37. Young J:** Naam.., Ezra tupe dakika moja tutakuwa tumefika. Twendeni haraka mashoga wangu…. **SASA HIVI**!

**38. Charlie:** Sasa twende haraka haraka vipi? Wewe unaendesha beskeli na sisi tunatembea!.

**39. Young J:** Eh, munaweza kunifuata mbio kama watu wanaofukuza mbuzi aliyeshikwa na kichaa.

**40. Sister P:** Young Junior, kabla ya kujifanya kuwa mbuzi

Mwenye kichaa, studio ya Ezra iko umbali gain?

**41. Young J:** Hapa karibu tu kwenye ule mlima…!

**42. Sister P:** Siwezi …! hata munifunge kwa kamba…!

**43. Young J:** Hebu twende Sister P, ni mwendo wa dakika moja tu. Twende. Ezra anasema fundi wa mitambo ana kazi nyingi na tunapaswa kufika haraka!

***SFX:*** ***(Desks being pushed, bicycle bell rings, kids screaming and laughing)***

**SCENE 2**

***SFX: A Path from the youth centre to the recording studio, sounds of nature: afternoon. Sister P and Charlie breathing very fast, confused footsteps, once in a while sticks are broken, a bicycle's chain is constantly heard and the bell clinging.***

**44. Charlie:** (***breathless***) Huu ni upuzi. Ndio sababu nataka kuanzisha studio yangu haraka iwezekanavyo. Niweze kuimba nyimbo na kurekodi nyimbo zetu za acapella au kucheza muziki wa kisasa na kukuza vipawa vyetu..!

**45. Sister P:** Nadhani televisheni ni bora zaidi,kwani unaweza kusikiza na pia kutazama kinachoendelea. Pia Televisheni inatoa fursa kwa watu kama wewe Young Junior kuonyesha vipawa vya katika kusakata ngoma mtindo wa ***break dance!***

**46. Charlie:** (***from a distance)*** Kwani tusishirikiane kuanzisha Gazeti. “Ama hutaki kuchemsha bongo za watu”?

**47. Sister P:** Sasa tuko umbali gani kufika Studio hiyo, Young J?

**48. Young J**:***(From a distance***) Si mbali sana,Sister P,.. Si mbali kabisa!

| | |
|---|---|
| ***SFX:*** | ***(Mobile phone rings)*** |

**49. Young J**: Hellooooooo….ndio, Ezra!

**50. Ezra:** ***(unclear voice on phone***) Young Junior!

**51. Young J:** Naam , Ezra…zungumza kwa sauti, siwezi kukusikia vizuri!.

**52. Ezra:** Unaweza kuwaambia rafiki zako waje wakati mwengine, kwasababu fundi wa mitambo amebadili nia..

**53. Young J:** ***(almost in a whisper)*** Sasa huo ni upuzi mtupu!. Ezra! ***(calling with begging command***)

**54. Ezra:** Eti fundi wa mitambo ana kazi nyingi sasa? .

**SCENE 3**

| | |
|---|---|
| ***SFX:*** | ***Outside the recording studio some soft choir music is heard in the background. It is at the road side and once in the while motorbikes and cars are heard passing by.*** |

**55. Young J:** Siwezi kuwaambia rafiki zangu habari hizi… Wataniua! .…

| | |
|---|---|
| **SFX:** | ***sounds of breathless sister P and Charlie, hurried footsteps*** |

**56. Young** Huyu ni Ezra..!, Ezra hawa ni wanachama wenzangu katika klabu ya *Dot.Com.*.

**57. Ezra**: *Dot.Com.Club*? Jina zuri sana . Ni vizuri kukutana nanyi . Lakini ningependa kuwaomba msamaha!.

**58. Sister p:** Ohh.., hakuna neno. Sisi ndio tunaopaswa kukuomba msamaha kwa kukucheleweshа

**59. Ezra:** Hata, mumefika wakati muafaka.Lakini samahamani fundi wa mitambo ameanza kazi nyingine, kwa hivyo hatuna budi kuahirisha mpangilio huu.

**60. Charlie:** Eti nini ?

**61. Sister P**: Siamini ! Young Junior!.

**62. Young J:** Usinitazame hivyo, Sister P. Huu sio mwisho…!

**63. Sister P:** Tosha…! . sitaki tena mimi nimejindoa. Nitajiimbia mwenyewe tu!.

**64. Ezra:** Hata sio hivyo.Bado wewe ni kijana!. Usikate tamaa haraka hivyo.. si vizuri. Hata mimi pia mambo si rahisi kwangu … nakujikakamua tu…!

**65. Charlie:** Lakini si umefaulu kutimiza ndoto yako?

**66. Ezra:** Angalau sasa nafurahia kile ninachofanya, yaani mwanafunzi katika sekta ya habari. Nyinyi Je? Munajua mnachotaka maishani?

**67. Charlie:** **N**doto yangu ni kuanzisha kituo cha redio, kucheza muziki moto moto mchana kutwa.Kwani inavyoonekana na kwamba shughuli za klabu hii sasa zinaelekea kugonga mwamba. Kituo changu nitakiita ***DOT COM FM STEREO.***

**68. Sister P**: Na sasa kwasababu mambo hayaendi vizuri , nataka kuelekeza juhudi zangu katika sekta ya televisheni, yaani niweze kuwahoji wasichana wenye vipawa vya aina mbali mbali na kuandaa mijadala kuhusu maisha ya wasichana wa rika langu!.

Haya yote hutaweza kuyasikia katika redio ya taifa.Na kipindi hicho kitafahamika kama … ***THE ME IN ME***… ama hivi ndivyo nitakavyoanza ***(clears her throat***) *" Huyu ni Sister P, kipenzi chako…!*

**69. Young J:** ***DRILL THE BRAINS*** ndilo gazeti la ndoto yangur. "Kutana na mhariri mkuu "Young Junior!"

| | |
|---|---|
| ***SFX:*** | ***Thunder and windy air*** |

**70. Ezra:** Kuna dalili ya kutanyesha leo ... lakini ajabu ni kwamba redio ya taifa imetangaza kutakuwa na jua mchana kutwa!

**71. Sister P, Charlie, Young J: J**e unayasikia hayo, Ezra?

**72. Ezra:** Ni kweli. redio ya taifa haisemi ukweli kabisa kuhusu hali ya hewa. Na fikra zenu ni nzuri!. Lakini naamini kuwa ushirikiao wenu ni bora zaidi kuliko mawazo ya mtu mmoja.Mnapaswa kukaa chini pamoja kushauriana na kisha kukubaliana kitu kimoja. Redio ni haraka, na haina gharama

kuanzisha. Kuanzisha kituo cha televisheni ni gharama kidogo na ni wachache walio na televisheni miongoni mwa jamii yetu.

**73. Young J:** Kwa hivyo tunaweza kuanzisha gazeti, kwa vile habari zinaweza kuhifadhiwa kwa muda mrefu kadri upendavyo

| | |
|---|---|
| ***SFX:*** | ***Thunder and windy air*** |

**74.Charlie:** Hiyo itategemea jinsi unavyolihifadhi.Iwapo italihifadhi katika nyumba ya Babako iliyoezekwa kwa nyasi na inaponyeshewa bila shaka litaharibika.

**75.Ezra:** Mandishi hudumu muda mrefu…lakini kama nilivyo tangulia kusema,nitafikiria suala hilo. Tulizungumzie suala hili la vyombo vya habari kwa kina zaidi wakati mwengine. Mvua karibu itanyesha leo usiku

| | |
|---|---|
| **SFX:** | ***(Rain fall)*** |

**END EPISODE**

**OUTRO**

Na hadi hapo tunafika mwisho wa makala haya ya kwanza katika mfululizo wa vipindi vyetu kuhusu Habari na vyombo vya habari.

Je Sister P ataendelea na mpango wake wa kuanzisha kituo cha Televisheni? Na je wana Dom.Com watafanikiwa katika juhudi za kutaka muziki wao uchezwa katika kituo cha redio ya Taifa?
Ungana nasi tena kwa makala mengine wakati mwengine ujue nini yatakayojiri. Na iwapo ungependa kusikiliza tena makala haya,unaweza kutembelea mtandao wetu Dw-world.de/lbe
Hadi wakati huo basi .. Kwaheri kwa sasa .